

**MUHTASARI WA KIKAO CHA WAKUU WA IDARA KILICHOFANYIKA TAREHE  
08/10/2021 KATIKA OFISI YA HALMASHAURI YA MJI.**

**Waliohudhuria**

1. Ndg. Hassan Kiseto	-Kaimu Mkurugenzi	-	M/Kiti
2. Ndg. Sekela Mwasubila	- Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA	-	Mjumbe
3. Ndg. Annette T. Nara	- Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari	-	"
4. Ndg. Fatuma Mwasingo	-Kaimu Mkuu wa Idara ya Ardhi na Maliasili	-	"
5. Ndg. Musa Kimwaga	- Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi	-	"
6. Dkt. Florence Hilari	- Kaimu Mkuu wa Idara ya Afya	-	"
7. Ndg. Alfred Chakalike	- Kaimu Mkuu wa Idara ya Mazingira	-	"
8. Ndg. Monica Kimario	- Mkuu wa Idara ya Mifugo na Uvuvi	-	"
9. Ndg. Irene Moshia	- Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii	-	"
10. Ndg. Magreth Dodo	-Kaimu Mkuu wa Idara ya Ujenzi	-	"
11. Ndg. Ziada Kassimu Musa	- Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Sheria	-	"
12. Ndg. Magreth C. Segu	- Mkuu wa Kitengo cha Uchaguzi	-	"
13. Ndg Rosemary Kimboi	- Kaimu Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara	-	"
14. Ndg. Thecla Nyoni	-Mkuu wa Idara ya Mipango, Takwimu na ufuatiliaji	-	"
15. Ndg. Pepino Mfugale	-K/Mkuu wa Idara ya Utumishi na Utawala		Katibu

**Sekretarieti**

1. Rosemary M. Mnguli - Mwandishi wa Vikao

**MUHT NA. 1/2021/2022 KUFUNGUA KIKAO**

Mwenyekiti alifungua kikao saa 7 : 30 Mchana baada ya kujiridhisha kuwepo kwa akidi ya Wajumbe.

**MUHT NA. 2/2021/2022 KUTHIBITISHA AGENDA ZA KIKAO**

Agenda zifuatazo zilithibitishwa na wajumbe na zilikubaliwa kujadiliwa

1. Kufungua kikao.

2. Kuthibitisha agenda za kikao.
3. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa kikao cha tarehe 17/09/2021
4. Yatokanayo na kikao kilichopita cha tarehe 17/09/2021
5. kupokea na kujadili taarifa za kamati za kudumu na zisizo za kudumu za Halmashauri.
  - I. Kamati ya Uchumi, Elimu na Afya.
  - II. Kamati ya mipango Miji na Mazingira.
  - III. Kamati ya kudhibiti Maambukizi ya VVU na UKIMWI
  - IV. Kamati ya Fedha na Utawala
6. Mapokezi ya fedha za UVIKO 19 kiasi cha Shilingi 460,000,000/= kwa ajili ya Ujenzi wa madarasa, Kiasi cha Shilingi 300,000,000/= kwa ajili ya ujenzi wa jengo la dharura Hospitali ya Halmashauri ya Mji Kondoa, Kiasi cha Shilingi 90,000,000/= kwa ajili ya ujenzi wa Nyumba ya Mtumishi (3 in 1) katika Kituo cha Afya Serya na kiasi cha Shilingi 500,000,000/= fedha za Tozo kwa ajili ya miradi ya Ujenzi.
7. Mengineyo
8. Kufunga kikao.

**MUHT. NA.3/2021/2022 MAPOKEZI YA FEDHA ZA UVIKO 19 KIASI CHA SHILINGI 460,000,000/= KWA AJILI YA UJENZI WA MADARASA, KIASI CHA SHILINGI 300,000,000/= KWA AJILI YA UJENZI WA JENGO LA DHARURA HOSPITALI YA HALMASHAURI YA MJI KONDOA, KIASI CHA SHILINGI 90,000,000/= KWA AJILI YA UJENZI WA NYUMBA YA MTUMISHI (3 IN 1) KATIKA KITUO CHA AFYA SERYA NA KIASI CHA SHILINGI 500,000,000/= FEDHA ZA TOZO KWA AJILI YA MIRADI YA UJENZI**

Mkuu wa Idara ya Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji aliwasilisha taarifa inayohusu mapokezi ya fedha za uviko 19 kiasi cha shilingi 460,000,000/= kwa ajili ya ujenzi wa Madarasa, kiasi cha shilingi 300,000,000/= kwa ajili ya ujenzi wa jengo la dharura Hospitali ya Halmashauri ya Mji Kondoa, kiasi cha Shilingi 90,000,000/= kwa ajili ya ujenzi wa Nyumba ya Mtumishi (3 in 1) katika kituo cha afya Serya na kiasi cha shilingi

500,000,000/= fedha za tozo kwa ajili ya miradi ya ujenzi ambazo zinahitaji utekelezaji wa haraka ili kufikia malengo ya fedha hizo.


Wajumbe walipokea na kuridhia taarifa hiyo kisha kushauri kuwa mchakato wa kuanza kwa miradi hiyo ufanyike mapema..

Aidha walishukuru kupokea fedha hizo ambazo zitatumika kwenye miradi husika iliyokusudiwa kwa ajili ya maendeleo ya Halmashauri ya Mji Kondo. Wajumbe waliipokea taarifa hiyo na kuridhia matumizi ya fedha hizo kwa hatua zaidi za kiutekelezaji.


#### MUHT NA. 4/2021/2021 KUFUNGA KIKAO.

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe wote kwa michango yao mizuri ya mawazo, aliwatakia safari njema warejeapo majumbani mwao. Alifunga kikao saa 2:00 usiku.

U m e t h i b i t i s h w a .



Jina LUCY J. TINUBA  
Katibu



Jina .....  
Mwenyekiti

08/10/2021

Tarehe